

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



• ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA NNE

01 SEPTEMBER, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA NNE – TAREHE 01 SEPTEMBER, 2023

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

45. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itaboresha mafao ya Wastaafu kwa kuongeza kiwango cha pensheni anayopata Mstaafu kwa mwezi.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

46. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, ni miradi mingapi ya kimkakati imejengwa katika Wilaya ya Illeje.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

47. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Mafuta ya Kula yanazalishwa kwa wingi nchini.

WIZARA YA KILIMO:

48. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha bei ya Zao la Mkonge haitetereki.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

49. MHESHIMIWA MAIDA HAMAD ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali italipa madeni ya fedha za kusafirisha mizigo kwa Askari Wastaifu.

50. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Vituo ya Polisi kwenye Kata za Mkiwa, Misughaa, Mungaa pamoja na nyumba za Askari Singida Mashariki.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

51. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK (TUMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, lini Serikali itawaendeleza Wavuvi kwa kuanzisha uvubi unaotumia dira maalum inayoelekeza Samaki walipo.

WIZARA YA AFYA:

52. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mkakati gani wa kumaliza upungufu wa Madawa na Vifaa Tiba katika Hospitali zetu nchini.

53. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini Serikali isiwekeze fedha kwenye Kiwanda cha Viuwadudu Kibaha ili kutokomeza Malaria nchini.

WIZARA YA FEDHA:

54. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, hatua zipi zimechukuliwa kuhusu Itifaki ya Forodha kati ya Tanzania na DRC baada ya DRC kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**DODOMA
01 SEPTEMBER, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**